Government of **Western Australia**
**Mental Health Commission**

**Una haki za:**

- kupokea maelezo kuhusu haki zako na haki za mtu unayemsaidia
- kupata maoni yako kufikiriwa na wafanyakazi
- kujulishwa matukio yanayolazimu kujulishwa
- kuhusishwa, na kupokea maelezo kuhusu, matibabu na utunzaji wa mtu unayemsaidia
- kutafutwa maoni kabla ruhusa inakubaliwa kwa mtu unayemsaidia
- kuomba maoni mengine kwa ajili ya mtu unayemsaidia
- kupokea maelezo kuhusu mipaka yoyote ya uhuru wa wasiliano ya mtu
- siri katika mazungumzo na wafanyakazi
- kuomba ukaguzi wa hali ya mgonjwa kuwa asiyekusudiwa kutoka Baraza ya Afya ya Akili (s: 08 6145 3900)
- kujulishwa kuhusu maombi kwa, na usikilizaji wa, Baraza ya Afya ya Akili
- kupata maoni yako kusikilizwa katika mambo mbele ya Baraza ya Afya ya Akili
- kuwakilisha mtu, au kuwakilishwa mbele ya Baraza ya Afya ya Akili
- kutoa malalamiko kwa huduma ya afya ya akili au Ofisi ya Malalamiko ya Huduma za Afya na Ulemavu (HaDSCO) (s: 1800 813 583) kama hufurahi.

## Maelezo zaidi

Maelezo katika brosha hii inahusisha masheria ambayo yamo Sheria ya Afya ya Akili 2014. Maelezo kuhusu Sheria hii imefupishwa katika seti ya brosha zifuatazo:

- Kupendekezwa kwenda kwa mtaalum wa magonjwa ya akili kwa uchunguzi
- Maagizo ya matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa hospitalini
- Maagizo ya matibabu ya jamii
- Maelezo kwa wagonjwa wa hiari
- Kupokea matibabu kwa ugonjwa wa akili
- Maelezo kwa watu wanaosaidia kibinafsi
- Watu walioteuliwa: Jinsi ya kuteua na maana kwake.

### Brosha zingine zinapatikana kutoka:

- Baraza ya Afya ya Akili
- Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili
- Kituo cha Sheria ya Afya ya Akili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Sheria ya Afya ya Akili 2014 na nyenzo zingine, angalia tovuti ya Tume ya Afya ya Akili: www.mhc.wa.gov.au au pigia simu (08) 6272 1200

This document can be made available in other languages and alternative formats on request.

Published by the Mental Health Commission (2015)

# Maelezo kwa watu wanaosaidia kibinafsi



Ukiwa wewe ni mtunzaji, mwanafamilia wa karibu, mzazi, mlezi au mtu aliyeteuliwa wa mtu anayepokea matibabu kwa ugonjwa wa akili, unaweza kuwa ‘mtu anayesaidia kibinafsi’.

Brosha hii inakutolea maelezo kuhusu wajibu yako pamoja na haki zako.

## Nani ni mtu anayesaidia kibinafsi?

Wewe unatambuliwa kuwa mtu anayesaidia kibinafsi wa mgonjwa kama wewe ni:

- mtunzaji wake (mtu ambaye halipwa na anatoa utunzaji wa kila mara kwa mgonjwa)
- mwanafamilia wake wa karibu (ndugu anayetoa utunzaji wa kila mara kwa mgonjwa)
- mzazi au mlezi wake wa mtoto
- mlezi au mlezi wake wa kudumu wa mtu mzima
- mtu aliyeteuliwa wake (mtu ambaye mgonjwa anateua rasmi kutumia Fomu 12A).

## Una wajibu gani?

Unastahili kuhusisha na matibabu na utunzaji wa mtu unayesaidia, pamoja na:

- kufikiria uchaguzi kwa matibabu na utunzaji,
- kumpa msaada kwa mtu, na
- kuandaa na kukagua matibabu, msaada na mpango wa kuruhusu kutoka hospitali.

Unaweza kuwajulisha wafanyakazi kiasi gani unachotaka kuhusika.

Ni muhimu kwamba unaposaidia mtu yule, uheshimu pia uzoefu na ubingwa wa wafanyakazi wa afya ya akili. Watu wanaosaidia wabidhii kufahamishwa vizuri na wote mgonjwa na wafanyakazi ili maoni sawasawa yanaweza kufikiwa.

## Utapata maelezo gani?

Kama mtu anayesaidia kibinfasi unastahili kupata maelezo yafuatayo kuhusu mtu unayemsaidia:

- ugonjwa wa akili unaotibiwa, uchaguzi kwa matibabu, na jibu kwa matibabu yoyote yanatolewa,
- sababu ambazo zinachangia kwa agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa hospitalini au agizo la matibabu ya jamii,
- hali yoyote iliyobidii kumtenga au kutumia kuzuia ya kimwili, na
- huduma zinazopatikana kuridhisha mahitaji yake.

Wafanyakazi watabidii ya kutosha kuwasiliana nawe, na/au mtu mwengine anayesaidia kibinafsi ili kukupa maelezo hayo. Kama mtu ambaye unamtunza ana watunzaji wengi na watu wengine wanaosaidia kibinafsi, mmojawapo anaweza kuwahi kupewa maelezo hayo.

## Wakati gani unaweza kutofahamishwa au kutohusishwa?

Kwa jumla, mgonjwa wa hiari anaweza kuamua kama anakubali au la kwa watu wanaomsaidia kibinafsi kufahamishwa au kuhusishwa. Hata hivyo, kama mgonjwa wa hiari hana afya nzuri ya kutosha kuweza kuamua uamuzi huu, utafahamishwa/husishwa isipokuwa kama kufanya hivyo sio kwa faida nzuri za mgonjwa

Katika visa vingi wafanyakazi watawafahamisha na kuwahusisha watu wanaosaidia kibinfasi wa mgonjwa asiyekusudiwa. Mambo ya pekee ni:

- Kama sio kwa faida nzuri za mgonjwa asiyekusudiwa; au
- Kama mgonjwa asiyekusudiwa hakubali kwa wewe kufahamishwa au kuhusishwa, na mtaalum wa magonjwa ya akili anaamua kwamba anaweza kuamua uamuzi huu na unaeleweka.

## Matukio yanayolazimu kujulishwa

Kuongeza kwa haki zako zingine ufahamishwa/husishwa, angalau mtu mmoja anayesaidia kibinafsi lazima afahamishwa kila wakati ‘matukio yanayolazimu kujulishwa’ yoyote yafuatayo yanatokea kwa mtu unayesaidia:

- agizo la kufunga, agizo la matibabu ya mgonjwa wa kulazwa hospitali au agizo la matibabu ya jamii, likifanyika, likifutwa (likibatilisha), au likiisha
- agizo lolote lingine linalofuata uchunguzi wa mtaalum wa magonjwa ya akili, likifanyika
- akiruhusu kuondoka baada ya kufungwa
- agizo la usafiri linafanyika
- anahamishwa kutoka hospitali moja kwenda zingine
- hayupo bila ruhusa, anapewa ruhusa kutoka hospitali au ruhusa yake inarefushwa, inabadilishwa au inafutwa
- alipewa matibabu ya haraka yasiyo ya afya ya akili wakati ana agizo la matibabu ya mgonjwa aliyelazwa hospitalini.

Wewe (au mtu mwengine anayesaidia) atafahamishwa kuhusu matukio hayo, hata kama mtu unayemsaidia hakubali. Mambo ya pekee ni inapokuwa sio kwa faida nzuri za mtu, au ingawa wafanyakazi wamejitahidi, wameshindwa kuwasiliana na mtu yeyote.